# HUDUMA ZA SERVISI ZINAZOTOA MSAADA WA AFYA NA USHAURI NCHINI NORUVEJE

**NAV**

- Ofisi za NAV zinafanyiwa ndani kazi na wafanyakazi wa kijami(wanasosholojia), wanasayansi wa kijamii, wanasheria, wenye wanahusikana na watu, wachumi wa kipesa,watu ambao wanapana elimu, na wengine wenye wanatumika na chuo kikuu(universitet) na asili ya(chanzo ya) chuo kikuu. Ofisi za NAV zinafanyiwa ndani kazi na wadaktari wa kunyoosha mishipa na mifupa(physiotherapy), wataalimu wa kazi za wakati wote, mtafsiri wa lugha ya kiziwi ambao hawasikii vizuri masikioni, mafundi wa kazi, wadaktari wa macho, watu ambao wanapana elimu ya kuona, waandishi wa sauti ,na watu ambao wanapana elimu ya wakusikia.
- Faida ya ukosefu wa kazi ya malipo ikiwa hauna kazi au unaachishwa kazi, malipo ya wagonjwa, faida za familia, msaada wa kiuchumi, habari, ushauri na mwongozo kwa kupata maelezo, mpango wa kuhitimu, ushauri wa kutumikisha pesa, na ushauri wa madeni, sehemu ya kuishi muda mfupi.

**Shule**

**Shule ya watoto wadogo**

**Usaidizi (huduma) wa afya ya shule(mstari wa 1)**

- Muuguzi wa afya(daktari msaidizi), daktari wa shule, daktari wa kunyoosha mishipa na mifupa(physiotherapy), mwanasaikolojia wa mafikiri, mwenye anahusikana na kuongea maneno ya kuhutubia.
- Mtihani wa kuanza shule(katika mwaka wa 1 wa shule ya msingi), kufundisha katika vikundi, na madarasa ya masomo  ya mambo mengine, afya ya kimwili, kiakili na ya kingono(kijinsia), mazungumzo ya afya katika mwaka wa 8, kupima uzito, chanjo, kuacha shule.

**Mahali cha afya ya watoto(mstari wa 1)**

- Usaidizi wa bure kwa watoto kati ya miaka 0 mpaka 5
- Muuguzi wa afya (mtu wa kukwangalilia na kukusaidia), daktari na daktari wa kunyoosha mishipa na mifupa(physiotherapy)
- Kutembelewa nyumbani mara 1, uchunguzi uliopangwa mara 13, mitihani mara 4 ya matibabu iliopangwa, chanjo, na mwongozo wa wazazi

**Mahali ya afya ya wavijana**

- Usaidizi wa bure kwa watoto kati ya miaka 13 na 23(25)
- muuguzi wa afya(mtu wa kukwangalilia na kukusaidia), daktari
- kupanga uzazi,kuonelea mimba, kutoa mimba, matatizo ya kula, huzuni, wasiwasi, upweke, mahusiano magumu ya familia, dawa za kulevya, unyanyasaji, vurugu,  na kuonelea

**STAT-PED**

- Huduma ya usadizi wa serikali kwa komine na kaunti katika kazi zao ili kutoa

Mafundisho tofauti kwa watoto na wanafunzi wenye matatizo ya kuona au kusikia, kupatikana uharibifu wa ubongo, kupoteza hisia pamoja, lugha ya ishara, na mawasiliano mbadala na ya ziada (ASK) na katika hali ngumu hasa katika maeneo ya masomo za shida ya kujifunza lugha na matatizo ya lugha/ hotuba.

- kuelekezwa na wahudumu wa afya

**PPT**

- Wanasaikolojia wa mafikiri, waelimishaji, watu ambao wanapana elimu maalumu ya kipekee, wafanyakazi wa jamii, wataalamu wa hotuba ya kuongea, walimu wenye mahitaji maalum ya kipekee
- kusaidia shule za chekechea za watoto wadogo na shule zenye uwezo na maendeleo ya shirika, na usaidiziwa mahitaji ya watoto na wanafunzi
- Imerejelewa na wazazi/walinzi, shule za chekechea za watoto, shule, kituo cha afya, vifaa vya msaidizi vya komine,BUP, daktari

**Huduma ya kazi na kunyoosha mishipa na mifupa(physiotherapy)**

- Watu wenye walisomea kazi ya kunyoosha mishipa na mifupa na viungo.
- Kuzuia, matibabu, mafunzo na mwongozo kwa watu wanaohitaji msaada wa kutunza au kuboresha uwezo wao wa kazi, mpangilio na urekebishaji wa misaada

**Maisha ya afya na kituo cha hedhi ya kutoka damu ya kike**

- Ni msaada wa kiheshima na wafanyakazi wana uzoefu tofauti za kimasomo, kama vile:matibabu ya mwili, malisho bora, ufundishaji, matibabu kwa kazi, uuguzi wa mtu wa kukwangalilia na kukusaidia, sayansi ya afya ya umma na saikolojia.
- Masomo mbalimbali ya teknolojia na za kimwili na shughuli ambazo kila mtu anaweza kushiriki, na pia inasaidia wazee, watu wenye hawana uwezo wa kusikia na au macho kutoona na kupoteza kusikia.

**Ulinzi wa mtoto**

- Wafanyakazi wenye elimu katika masomo ya shughuli, maadili inayokubaliwa, sheria, ufundishaji, saikolojia na sayansi ya jamii.
- Usaidizi wa serikari kwa mtoto kwanza zitatoa msaada na usaidizi, ili wazazi wenyewe waweze kuwapa watoto wao utunzaji mzuri. Msaada na usaidizi unaweza kwa mfano kuwa ushauri na mwongozo kwa wazazi, usaidizi wa kuonelewa nyumbani mwishoni mwa wiki, kutembelea nyumba, makundi ya wazazi, msaada mawasiliano au msaada kwa ajili ya shughuli za kujifurahisha.

**Huduma za servisi za shida za maisha**

- Wauguzi wanaosaidia watu wenye magonjwa ya akili na wafanyakazi wa kijamii walio na mafunzo zaidi ya kazi ya afya ya akili.
- Usaidizi wa bure kwa watu walio katika mashida mengi ya maisha, kwa mfano matukio makubwa ya maisha kama vile ajali, kupoteza watu wa karibu kupitia kifo cha ghafla au kujiua, kuishi pamoja au kuachana. Wanatoa mazungumzo, ushauri na usaidizi wa kujisaidia.

**Idara ya ajali na Dharura (mstari wa 1)** (ikiwa kuna hali mbaya)

- Idara ya ajali na dharura ya Bergen inakubali wagonjwa wanaohitaji usaidizi ya haraka ikiwa kuna ugonjwa mkali au majeraha( shida ambayo hukujitayarishia). Piga simu 116 117 kabla ya kwenda kwenye Kliniki ya ajali ya Bergen na dharura (haitumiki ikiwa utaenda kliniki ya majeraha).
- inafungua kila saa na kila dakika.

**Daktari anaye kuhusu(mstari wa 1)**

- Huyu ni daktari wa kwanza wa mgonjwa yako ambaye unapashwa kuzungumza naye kwanza. Yeye anaweza kufanya utambuzi kwa magonjwa ya mtu, au kuwaelekeza kwa uchunguzi na jinsi ya kupata matibabu hospitalini. Daktari wako anaweza kuandika maagizo na likizo ya kutoenda kazini kwa sababu ya magonjwa yako.

**Msaada wa watoto na familia**

- Wauguzi wa afya ya umma, wanasaikolojia, washauri wa familia
- Kusaidia watoto na vijana, ushauri kwa wazazi, huduma kwa wanawake wajawazito na msaada kwa wale wanaofanya kazi na watoto na vijana.

**Ofisi ya Ushauri wa Familia**

- Wanasaikolojia, waelimishaji, wanateolojia na wafanyakazi wa kijamii wenye elimu zaidi katika tiba ya familia
- kusaidia katika uhusiano, msaada kwa familia, kusaidia kushirikiana na watoto wa kawaida, msaada kwa watoto na vijana, usaidizi kwa wazazi walionyimwa ulinzi wa mtoto wao, upatanishi katika tukio la kuvunjika
- Kutoa ushauri, mwongozo, masomo na vikundi vya majadiliano

**Kituo cha Afya ya Uhamiaji (SEMI) (mstari wa 1)**

- Madaktari, wauguzi wa afya ya watu, wauguzi, wanasaikolojia, wafanyakazi wa kijamii, wafanyakazi wa mazingira, nk.
- Uchunguzi wa afya, kupima (tathmini) afya, na matibabu, mazungumzo, rufaa ya kufuatilia malamiko, na mengineyo

**Huduma za servisi ya afya ya wajuzi (mstari wa 2) / hospitali**

- Huduma ya servisi ya afya ya kitaalamu(kiujuzi) ni pamoja na hospitali za kusoma na akili, kliniki za wagonjwa wa nje na vituo vya matibabu, shirika za ukarabati na ukarabati, taasisi mbalimbali, matibabu maalum ya kiujuzi kwa matumizi mabaya ya dawa, huduma za prehospital, mazoezi ya kibinafsi,wasomi na kazi za wadaktari hupimia mitihani ya afya ya wagonjwa hospitalini(maabara) ya kupimia na X-ray ya kuchunguza kuvunjika kwa mifupa
- Huduma ya afya ya kisomi ya wadaktari, itatambua au kujua maabara, kutibu na kufuatilia wagonjwa wenye hali mbaya,magonjwa makubwa na ya muda mrefu na matatizo ya kiafya.

**Saikolojia ya watoto na vijana (BUP) (mstari wa pili)**

- Wanasaikolojia, waelimishaji wa kupana elimu, wafanyakazi wa kijamii kwa watu, madaktari, na wenginewo
- BUP inatoa tathmini na matibabu ya matatizo ya akili kwa watoto, vijana na familia zao

**Kituo cha Magonjwa ya Akili cha Wilaya (DPS) (mstari wa pili)**

- Wanasaikolojia, madaktari, wauguzi, wafanyakazi wa kijamii, wauguzi wasaidizi, wafanyakazi wa mazingira, na mengineyo
- Hutoa tathmini(vipimo) maalum ya kiujuzi na matibabu tofauti ya matatizo ya akili katika wagonjwa wa nje, mazingira ya wagonjwa au kama matibabu ya kila siku.

**Mshauri na mwalimu**

- Kushauri mtu mwenye ujuzi mwingi katika eneo ya sehemu fulani. Mara nyingi mtu hufanya kazi kwa vyama au wanasiasa(shirika). Mshauri ni maelezo ya kiujuzi kwa mtu ambaye hutoa utaalam wa ujuzi wao katika uwanja fulani kupitia ushauri au mwongozo.
- Mwalimu ni neno la pamoja kwa kila mtu anayefanya kazi na kufundisha, na inatumika kwa wale wote ambao wanafanya kazi katika shule za chekechea watoto wadogo, shule za msingi, shule za sekondari, shule za sekondari za watu na elimu ya watu wazima.

**Huduma ya afya ya kibinafsi**

- Kwa mfano, Volvat, Aleris, Drop in
- Ushauri wa kimwili au mtandaoni na mtaalamu wa jumla, mtaalamu wa matibabu, mwanasaikolojia, mtaalamu wa viungo,
- upasuaji wa plastiki, wataalamu wa mapambo, nk
- Uchunguzi wa kutunza magonjwa

**Ushauri wa mtandaoni (binafsi)**

- Kupitia mazungumzo au simu ya video na daktari, unaweza kupata ushauri wa matibabu, tathmini na matibabu ya magonjwa ya kuambukiza hayahitaji uchunguzi wa mwili.
- Daktari anaweza kuagiza vipimo vya damu, kumrejelea mtaalamu ya ujuzi, rudilia uchunguzi wa radiolojia ya vipimo vya afya, kuandika maagizo. Daktari hawezi kuchapisha likizo ya wagonjwa.

**Jumuiya ya Imani**

- Mashirika mengi ya kidini kama vile Misheni ya Jiji la Kanisa, Caritas, Jumuiya ya Kiislamu ya Bergen inatoa shughuli mbalimbali za burudani.

**Mashirika yasiyo ya kiserikali**

- Mashirika ya kujitolea ni mashirika yasiyo ya kiserikali yanayosimamiwa kwa kuzingatia juhudi za hiari za kutumika kazi bila mshahara. Wanatoa shughuli nyingi tofauti kwa watoto na watu wazima.
- Msalaba Mwekundu, Robin Hood Huset, ROS (Ushauri juu ya matatizo ya kula), maktaba ya Bergen.

**Mshauri wa Ujumuishaji (IK)**

Mtu wa mawasiliano ambaye atakusaidia kwa ushirikiano na makazi nchini Norveje.